

Tuungane pamoja kuwaangamiza inzi waharibifu wa miembe

Tambua tatizo

Maembe huoza kutokana na viwavi vya nzi wa miembe au nzi waharibifu viishivyo na kula ndani ya maembe. Nzi wa miembe ni mdudu mdogo mwenye mabawa ambaye ana urefu wa wastani wa sentimita moja. Wanafanana na nzi wa kawaida kimaumbile lakini wao ni wadogo zaidi, na wanarangi nzuri. Viwavi vyake ndani ya tunda huwa na rangi ya manjano nyeupe na wana urefu wa wastani wa milimita moja na hukaa kwa wingi.

Habari tangulizi

Nzi wa miembe hushambulia maembe machanga na hupenyeza mayai ndani ya matunda. Mayai huanguliwa na kuwa viwavi ambavyo hukuwa ndani ya matunda na hivyo kufanya iwe vigumu kuwaua. Viwavi hawa husababisha matunda kuoza na hivyo matunda hudondoka chini kabla ya kuiva. Baadhi ya matunda yaliyoshambuliwa hubaki kwenye miti lakini ubora wake unapungua. Nzi hawa huruka na kushambulia matunda mapya wakiongozwa na harufu ya matunda. Hukaa kwa wingi, hivyo zoezi la kuwazuiwa linaweza kufanikiwa kama litafanywa na jamii nzima ya wakulima wa miembe.

Usimamizi

Chukua chupa tupu ya plastiki ya maji yenye ujazo wowote na uikate nusu. Kipande cha juu hufanana na mpare.

- Jaza robo ya chupa na juisi ya maembe yenye chachu au ndizi iliyochacha. Juisi hii huwavuta nzi ambao huingia ndani ya chupa. Unaweza kuongeza ongeza matone 2-5 ya sumu ya kuua wadudu kulingana na ukubwa wa chupa inayotumika.
- Mchanganyiko huu ndani ya chupa utawaua nzi. Mpare hugeuzwa juu chini na kuwekwa kwenye kipande cha chupa kilichobaki. Kwa wastani mitego 10 huwekwa kwenye eneo la mita za mraba 100 (sawa na kiwanja cha mpira) na huni'ginizwa usawa wa matawi ya chini ya mti. Hii hufanyika kipindi kabla ya matunda kuanza.
- Njia hii itafanikiwa kama kila mmoja atashiriki hivyo ni vyema kupanga, kutengeneza na kutumia mitego hii kwa pamoja.

Juu, nzi wa miembe. (Picha na Georg Goergen)



Juu, chini kiwavi. (Picha na Maui Jungalow)



Wakati wa kutumia kemikali, vaa mavazi ya kinga wakati wote na ufuate maelekezo kwenye lebo ya bidhaa, kama vile kipimo, majira ya kuweka, muda kabla ya kuvuna

Jina la kisayansi > *Bactrocera spp. (Vidudu in Swahili)*

Mapendekezo katika vidokezo hivi yanatumika katika: Kenya, Tanzania, Uganda



WAANDISHI: L. K Mahoo, K. Mtembei, Mwangi Jubilant
PO Box 22, Lushoto
Simu: +255 787055853 Barua pepe: lkmahoo@yahoo.com

Mwisho na Plantwise